

Yahya Ali Omar. 1998. Three prose texts in the Swahili of Mombasa. Sprache und Oralität in Afrika, Band 21. Berlin: Dietrich Reimer Verlag. ISBN 3-496-02636-7.

Shaykh Yahya Ali Omar gilt als der hervorragendste Kenner des Swahili im heutigen Mombasa. Er hat die folgenden drei Prosatexte übersetzt: Die zwei ersten, 'Eine Fahrt durch den Himmel' (*Matembezi ya p'eponi*) und 'Eine Fahrt durch die Hölle' (*Matembezi ya motoni*), ernteten höchstes Lob, als sie zum ersten Mal in den fünfziger Jahren in Mombasa im Radio übertragen wurden. Im Laufe der Jahre ist 'Eine Fahrt durch den Himmel' mehrmals nachgedruckt worden. Der dritte Text des vorliegenden Bandes, 'Das Leben von Adam und Eva' (*Maisha ya Nabii Adamu na mwana Hawa*), ist ein Prosadialog. Für die Swahili Literatur war diese literarische Gattung Neuland. Der Dialog wurde später durch Mombasas führenden Dichter Abdilatif Abdullah in Verse gefasst, und ist in dieser poetischen Version weit bekannt, vor allem, weil es im ostafrikanischen Abitur auf dem Lehrplan für Swahili stand.

Es gibt zwar unzählige Veröffentlichungen, in denen man swahili Prosa sowohl in der standardisierten Sprache wie auch im Sansibar-Swahili studieren kann. Bis jetzt aber hat es nur wenige mit Anmerkungen versehene Prosatexte in Mombasa-Swahili (kiMvita) geben, und wenn, dann meistens nur in schwer erhältlichen Zeitschriften. Das Buch ist also das erste seiner Art, und vielleicht auch das letzte, denn der Mombasa-Dialekt wird schon seit mehr als fünfzig Jahren aus politischen, bildungsbedingten und anderen Gründen zurückgedrängt. Deshalb ist dieses Buch nicht nur ein Textbuch für Swahili-Studenten, sondern stellt auch gleichzeitig ein Sprachdenkmal der ganzen Bevölkerungsgemeinschaft dar.

Said S. H. Omar

Issa Nasser Issa Al-Ismaily. 1999. Zanzibar: Kinyang'anyiro na utumwa [Slavery and the Scramble for Zanzibar]. Ruwi (Oman). xlii + k'urasa 285.

Mila na dasturi za kiSwahili zimeendelea katika up'wa wa Afrika ya mashariki kwa kiyasi cha myaka elfu. Baadhi ya miji ya kiSwahili ishamalizika, kwa mfano Ngare (Port Reitz), na waNgare wenyewe hawako tena; na miji mingine imo katika khatari; na miji ya kiSwahili yenye tamaa ya kubakiya ni michache sana. Matatizo mengi ya waSwahili hivi sasa hakuna namna ya kuyataua, lakini baadhi ya matatizo yanaweza kutatuliwa. Tatizo moja ni kutoa vitabu vya kiSwahili vilivyotungwa na waSwahili. Kutoa vitabu kama hivyo katika siku za utawala wa waZungu ilikuwa sahali kuliko sasa. Katika kame ya wahedi wa ishrini ni vigumu kwa vijana katika miji ya uSwahilini kusoma juu ya tarekhe yao na mila yao na lugha yao. Maana kitabu kilichotungwa na jamaa yao kwa lugha yao lau chatokeya kitakuwa taabu k upatikana na pia kitakuwa ghali. Kwa bahati Sheikh Issa Al-Ismaily, ambaye sasa umri wake ni zaidi ya myaka sabiini, amewafanya wema mkubwa wasomaji wa kiSwahili kwa kutoa kitabu hichi kilichotungwa kwa kiSwahili cha

cha waziwazi, tena kilicho fasaha – hii ni nyongeza k'ubwa katika elimu ya terekhe, na Sheikh Issa ni wa kupawa tahniya kwa kazi yake.

Kitabu hichi kimegawanywa sehemu t'atu. Sehemu ya kwanza inakhusu kinyang'anyiro cha uSwahilini, hasa Unguja (k'urasa 1 – 99) na kinaeleza khabari ya wafaume wa kiBusa'idi walio-tawala uSwahilini kunaziya utawala wa Sayyid Sa'id bin Sulṭān mpaka utawala wa Sayyid Jamshīd bin 'Abdullāh na mapinduzi ya Ijumaa, 2 Ramadhani 1383 / 12 Januari 1964 (babake mtungaji alikuwa ni mmoja katika wat'u waliodhulumiwa roho zao wakati huo wa balaa k'ubwa). Jumla ya wafaume walio-tawala uSwahilini ni hidashaara (au ithnashaara pamoja na Sayyid Khalid bin Bargash aliyetawala kwa siku mbili tu katika mwaka 1314 AH / AD 1896).¹ Miongoni mwa wat'u waliokuja uSwahilini wakati wa utawala wa Sayyid Sa'id walikuwa waArabu na waHindi na maBanyani na waZungu (maMerikani na waNgereza na maFaransa na maJarumani) na wat'u wa bara. WaZungu walikuwa na nguvu katika muda huu. Kwa mfano, baada ya kufa Sayyid Sa'id (alikuwa baharini 1273 AH / AD 1856) waNgereza waligawanya dola ya maBuSa'idi katika sehemu mbili kuanziya mwaka 1277 AH / AD 1861 – sehemu ya Omani t'ini ya Sayyid Thuwaynī na sehemu ya Swahili t'ini ya Sayyid Majīd; na mwisho kabisa (yaani kabla ya mapinduzi ya 1383 AH / AD 1964), Sayyid Jamshīd alikubaliana na waNgereza katika mwaka 1383 AH / AD 1963 kutokuwa na haki yoyot'e juu ya mahmiya ya Kenya (yaani nt'i ya Swahili kutoka Vanga mpaka maGunyani).

Sehemu ya pili inakhusu harakati za siasa za Unguja na P'emba (k'urasa 101 – 142). Na Sehemu ya mwisho inazungumza kukhusu biashara ya utumwa na utumwa wenyewe (k'urasa 143 – 282). Mengi yameandikwa na waZungu juu ya biashara ya utumwa iliyofanyika Afrika ya mashariki. Lakini inatubidi kukumbuka waliyofanya waAfrika wenyewe katika biashara hii. Vilevile ni makosa makubwa kutokumbuka biashara ya utumwa katika Afrika ya magharibi. Kwa mfano Leopold wa pili, mfaume wa maBeljiki (*roi des Belges*) alifanya Kongo ni milki yake haswa (yaani *l'état indépendant du Congo*), na dhuluma na unyang'anyi wake haukuwa na kiyasi. Katika utawala wake inakadiriwa kuwa wenyeji katika Kongo walipungua milioni kumi. Na ni aibu k'ubwa kuwa waZungu wa misheni wa kikatholiki katika Kongo ya Leopold II hawakusema lolot'e juu ya mambo maovu waliyaona yakifanyika Kongo. Yaonesha kuwa waZungu katika Afrika ya mashariki waliona walio-taka kuliona – nyani haoni kundule!

Kabla ya kutia naga nataka kutaja makosa madogo madogo. Ramani ya 'dawlat Zinjibar' (ukurasa 4) haikuandikwa terekhe yake; tena katika kitabu kilichotungwa chot'e kwa kiSwahili yaonesha si sawasawa ramani iliyomo kutaja majina ya mawahali kwa kiZungu, kwa mfano 'Comoro islands' (badala ya maSiwani), 'Lake Victoria' (Ziwa la Viktoria), 'R[iver] Pangani' (mto wa

¹ Sayyid Khalid bin Bargash alikufa Mambasa 1345 AH / AD 1927, na alizikwa nde ya mskiti wa Shaikh Jundani. Picha yake imo katika: Kevin Patience, *The shortest war in history*, Bahrain 1994, ukurasa 8.

P'angani), na kadhalika. Katika 'Mapitio' (k'urasa 283 – 285) ni ajabu kabisa kuwa mtungaji hakutaja kitabu cha Sheikh Abdalla Saleh Farsy kukhusu Sayyid Sa'id.² Pia kitabu cha Hollingsworth kukhusu tarekhe ya p'wani ilikuwa yafaa ataje jina la tarjuma yake ya kiSwahili.³ Mwisho wa kitabu hakutiwa fahirisi – naʼumai itaongezwa katika ch'apa ya pili.

Makosa mengine ni kuwa kitabu hichi hakina nambari ya ISBN. Kwa hivyo itakuwa taabu kuki-agiza, na kwa hakika sijakiona katika duka lolote la vitabu Afrika ya mashariki wala Ulaya. Kinapatikana kwa Sheikh Issa Al-Ismaily mwenyewe, P.O. Box 2968, Ruwi, Postal Code 112, Sultanate of Oman.

P.J.L. Frankl

² a) Abdulla Saleh Farsy, *Sayyid Said Bin Sultan*, Zanzibar [1942?].

b) kimetarjumiwa kwa kiArabu: *Al BūSa ʿidūn: hukām Zanjibār*, Masqaṭ 1980

c) kimetarjumiwa kwa kiNgeresa (na J.W.I. Allen): *Sayyid Said bin Sultan: Joint Ruler of Oman and Zanzibar (1804 – 1856)*, New Delhi 1986.

³ L.W. Hollingsworth, *Historia fupi ya Pwani ya Afrika Mashariki*, London 1951